**08-Sajdatut-Tilaawah (Sijda Ya Kisomo)**

**سَجْدَةُ التّلاوَة Sajdatut-Tilaawah - Sijda ya Kisomo**

Hutegemewa kupatikana wakati wo wote ule ikiwa mtu atasoma Aayah yenye sijda iwe ndani ya Swalaah au nje. Unaposoma ukapitia Aayah yoyote ile yenye sijda unategemewa na inapendeza kusujudu; Huu ndio ulivyokuwa mwenendo wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na ndivyo inavyopendekezwa katika adabu za kusoma Qur-aan, kuitika kwa kutekeleza hicho inachokutaka Aayah, nacho ni kusujudu ambako kutaweza kuwa kama ni dalili ya kimatendo kwa kuonyesha unyenyekevu na utiifu kwa Allaah (سبحانه وتعالى) kama Anavyosema:

قُلْ ءَامِنُوا۟ بِهِۦٓ أَوْ لَا تُؤْمِنُوٓا۟ ۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْعِلْمَ مِن قَبْلِهِۦٓ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ لِلْأَذْقَانِ سُجَّدًا ﴿١٠٧﴾

**((Sema: "Iaminini au msiamini. Hakika wale waliopewa elimu kabla yake wanaposomewa (Qur-aan) wanaporomoka kifudifudi wanasujudu."))[1]**

Dalili kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم):

عَنْ ابْنِ عُمَرَ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا قَالَ كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقْرَأُ عَلَيْنَا السُّورَةَ فِيهَا السَّجْدَةُ فَيَسْجُدُ وَنَسْجُدُ حَتَّى مَا يَجِدُ أَحَدُنَا مَوْضِعَ جَبْهَتِهِ"

**Imepokewa kutoka kwa Ibn 'Umar** (رضي الله عنهما) **amesema: "Mtume** (صلى الله عليه وسلم) **alikuwa akitusomea Suwrah yenye sajdah, kisha husujudu nasi tunasujudu mpaka mmoja wetu hapati sehemu ya kuweka kipaji chake"[2]**

**Vipi kusujudu kwake:**

---

[1]Al-Israa (17: 107)
[2]Al-Bukhaariy

Utakapotaka kuleta سَجْدَة التّلاوَة (sajdatut-tilaawah) nje ya Swalaah utatakiwa ulete *takbiyrah* (useme: *"Allaahu Akbar"*) na kusujudu. Kisha utanyanyuka kutoka kwenye kusujudu bila ya kuleta *takbiyrah* wala kuleta salaam; na huwa ni sijda moja tu, ambayo anasujudu msomaji na msikilizaji kama wanavyosujudu sijda ya Swalaah kwa viungo vyake saba; [kuweka viganja viwili ardhini, vidole vikiielekea Qiblah, magoti mawili, na matumbo ya vidole vya miguu akijitahidi vidole vielekee Qiblah, na kipaji cha uso pamoja na pua (vikihesabika ni kitu kimoja) na ahakikishe kapanua viwiko vyake (asiibane mikono yake kwenye mbavu zake) na tumbo lisigusane na mapaja yake].

Ama ikiwa سَجْدَة التّلاوَة (sajdatut-tilaawah) katika Swalaah basi itawajibika kuleta *takbiyrah* kwa kusema: ***'Allaahu Akbar'*** wakati wa kusujudu na wakati wa kunyanyuka baada ya kusujudu kwani imethibiti kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akileta *takbiyrah* wakati wa kusujudu na wakati wa kunyanyuka kwenye sijda, na hii inakusanya sijda za Swalaah na سَجْدَة التّلاوَة (sajdatut-tilaawah) zilizo ndani ya Swalaah.

**Du'aa ya سَجْدَة التّلاوَة Sajdatut-Tilaawah :**

Katika kusujudu, iwe sijda ya Swalaah au ya kisomo, kinachotakiwa kusomwa ni *adhkaar* za sijda zilizothibiti kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kama zifuatazo:

**سُبْحانَ رَبِّيَ الأَعْلى**

***Subhaana Rabbiyal A'alaa*** [x3] [3]

**"Ametakasika Mola wangu Aliye juu "**

[3] Ahlus-Sunan, Ahmad, Swahiyh At-Tirmidhiy

**اللَّهُمَّ لَكَ سَجَدْتُ وَبِكَ آمَنْتُ وَلَكَ أَسْلَمْتُ سَجدَ وَجْهِي لِلَّذِي خَلَقَهُ وَصَوَّرَهُ وَشَقَّ سَمْعَهُ وَبَصَرَهُ تَبارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ**

***Allaahumma Laka sajadtu wa Bika aamantu wa Laka aslamtu, sajada waj-hiya liLLadhiy khalaqahu wa swawwarahu, wa shaqqa sam-'ahu wa baswarahau bihawlihi wa quwwatihi Tabaaraka-Allaahu Ahsanul-Khaaliqiyn[4]***

**"Ee Allaah, Kwako nimesujudu, na Wewe nimekuamini, na Kwako nimesilimu, umesujudu uso wangu kumsujudia Yule Ambaye Ameuumba na Akapasuwa masikio yake, na macho yake, kwa uwezo Wake na nguvu Zake, Amebarikika Allaah Mbora wa Waumbaji"**

Pia mtu anaweza kuongeza du'aa zozote mbalimbali azipendazo sehemu hiyo. Baadhi ya Wanavyuoni wamenukuu du'aa zifuatazo zinasomwa kwenye **سَجْدَةُ التّلاوَة** (sajdatut-tilaawah).

**سَجَدَ وَجْهي للَّذي خَلَقَهُ وَصَوَّرَهُ وَشَقَّ سَمْعَهُ وَبَصَرَهُ بِحَوْلِهِ وَقُوَّتِهِ ﴿ فَتَبَارَكَ ٱللَّهُ أَحۡسَنُ ٱلۡخَٰلِقِينَ ﴿١٤﴾ ﴾**

***Sajada wajhiya liLLadhiy khalaqahu, wa swawwwarahu, wa shaqqa sam-'ahu wa baswarahu bihawlihi wa quwwatihi, fa-Tabaaraka-Allaahu Ahsanul-Khaaliqiyn***

**Umesujudu uso wangu kumsujudia Ambaye Ameuumba na Akapasuwa masikio yake, na macho yake, kwa uwezo Wake na nguvu Zake, ((Amebarikika Allaah Mbora wa waumbaji))[5]**

**اللّهُمَّ اكْتُبْ لي بِها عِنْدَكَ أَجْراً، وَضَعْ عَنّي بِها وِزْراً، وَاجْعَلها لي عِنْدَكَ ذُخْراً، وَتَقَبَّلها مِنّي كَما تَقَبَّلْتَها مِنْ عَبْدِكَ داوُد**

***Allaahummak-tub-liy bihaa 'Indaka ajran, wa dhwa'a 'anniy bihaa wizran, waj-'alhaa liy 'Indaka dhukhran, wa taqabbalhaa minniy kamaa taqabbaltahaa min 'abdika Daawuwd***

---

[4] Swahiyh Muslim - *Kitaabu Swalaatil-Musaafiriyn*

[5] At-Tirmidhiy (1/90) na ameisahihisha Ibn Maajah (1/148)

**Ee Allaah niandikie Kwako kwa sajdah hii malipo, na nifutie kwayo madhambi, na ijaalie kwangu mbele Yako ni akiba, na nikubalie kama Ulivyomkubalia mja wako Daawuwd[6]**

## Idadi Ya سَجْدَةُ التّلاوَة Sajdatut-Tilaawah

سَجْدَةُ التّلاوَة (sajdatut-tilaawah) zilizothibitishwa katika Qur-aan ni kumi na tano[7]. Wanachuoni wamekubaliana na kushajiisha kuwa sijda ifanywe katika sehemu hizo zilizobainishwa kuwa ni za sijda kwa kuwekewa alama maalumu katika karibu misahafu yote, na hiyo سَجْدَةُ التّلاوَة (sajdatut-tilaawah) huwa ni *mustahabb* (jambo lenye kupendeza) kwani si sijda ya lazima[8].

---

[6]At-Tirmidhiy (2/473), Al-Haakim na ameipa daraja ya Swahiyh Adh-Dhahabiy (1/219)

[7] Wako Maulamaa wenye kuona kuwa *sajdatu-tilaawah* ni 14 tu kwa kuitoa sijda ya Suwrat Swaad; kwani wako wenye kuiona kuwa ni *sajdatu-tilaawah* na wako wenye kusema si *sajdatu-tilaawah*, kila upande ukiwa na dalili yake; na kilichothibiti kuhusiana na sijda ya Suwrah Swaad ni Hadiyth ya Ibn 'Abbas (رضي الله عنهما) kuwa : Si katika '*azaaimu sujuwd;* lakini amemuona Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisujudu sijda hii ya Suwrat Swaad. (rejea chini kwa majina ya Suwrah na nambari ya Aayah ambamo Muislamu anapaswa kusujudu anaposoma au kusikia zikisomwa) .

[8]Inatakiwa ifahamike kuwa kitendo cha *mustahabb* (kupendezwa kufanya) hakina hadhi sawa na faradhi lakini ni miongoni mwa namna ya kujipendekeza na kujikurubisha kwa Allaah (سبحانه وتعالى) na Muislamu mzuri ni yule anaetafuta kila njia ya kujikurubisha na kujipendekeza kwa Allaah (سبحانه وتعالى) na hakuna wakati mja yu karibu zaidi na Allaah (سبحانه وتعالى) kuliko anapokuwa katika *sujuwd;* hivyo kuiacha sijda ni kujikosesha kuwa karibu na Mola kitu ambacho ni muhali wala hakiingia akilini, kwani hicho ndio anachokitafuta kila mwenye kuamini Allaah na Aakhirah, na kuiacha kwa makusudi inaweza ikaeleweka kama ni dharau kwani jambo lililothibiti kufanywa au kuletwa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) katika Hadiyth zilotajwa Mlango huu; (i) kutoka kwa Ibn 'Umar (ii) Kutoka kwa 'Abdullaah kupitia kwa Al-As-wad (iii) Kutoka kwa Ibn 'Abbaas kupitia kwa 'Ikrimah (رضي الله عنهم) zilorekodiwa na Al-Bukhaariy. Kwa hiyo haifai kwa Muislamu khasa yule anaependa kuisoma Qur-aan au kuisikiliza kama alivyokuwa akiisoma na kuisikiliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuacha kutenda amali kama hii, hata kama kutakuwa kuna kauli gani ya Maulamaa maadam imethibiti kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) basi isiachwe, vyenginevyo kuna hatari ya mtu kwa kuliacha kabisa kukosa kheri nyingi bali kuwa ni mkosa.

**Je inahitaji Twahaarah?**

Kwa kuwa sijda ni miongoni mwa matendo maalumu na hasa yanayohusiana na yaliyomo katika Swalaah ambayo katika sharti lake kubwa ni kuwa na *twahaarah*. Na ingawa Wanachuoni wengi wanaonelea kuwa mwenye kutaka kusujudu سَجْدَةُ التّلاوَة (sajdatut-tilaawah) inampasa awe na udhu kwa hoja kuwa masharti ya Swalaah ndiyo masharti ya sijda hiyo, lakini kauli iliyo sahihi kabisa ni kuwa سَجْدَةُ التّلاوَة (sajdatut-tilaawah) haina hukmu ya Swalaah; hivyo basi msomaji na msikilizaji wa Qur-aan wakipita katika Aayah yenye kutajwa sijda itapendeza kusujudu hata kama hawana udhu[9]. Na huu ndio msimamo wa Ibn 'Umar (رضي الله عنه). Dalili pia ni Hadiyth zifuatazo: ambazo zinaeleza kwamba hata makafiri walisujudu iliposomwa Aayah yenye sijda

**عَنْ عِكْرِمَةَ عَنْ ابْنِ عَبَّاسٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ سَجَدَ بِالنَّجْمِ وَسَجَدَ مَعَهُ الْمُسْلِمُونَ وَالْمُشْرِكُونَ وَالْجِنُّ وَالْإِنْسُ**

**Imepokewa kutoka kwa 'Ikrimah kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهما) kwamba: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisujudu aliposoma Suratun-Najm na wakasujudu pamoja naye Waislamu, washirikina, majini na watu"[10]**

---

[9]Imaam Ibn Hazm, Shaykhul-Islaam Ibnu Taymiyah, Imaam Al-Bukhaariy na Ash-Sha'aby wanatoa hoja ya kuwa haiwezi kuwekewa sharti ya *twahaarah* kwa sababu سَجْدَةُ التّلاوَة (sajdatut-tilaawah) si Swalaah na khasa ukichukulia kuwa asiye na udhu anaruhusiwa kusoma Qur-aan na kisomo chake kinajuzu, na kama hali ndio kama hiyo basi huwa anapita kwenye Aayah zenye sijda na bila shaka atapenda kusujudu kama alivyopenda kuisoma Qur-aan na wakati huo kumtaka kunyanyuka na kutia udhu kwa kuwa kasoma Aayah yenye sijda ni kumkalifisha na hilo halijawahi kupokewa katika mapokezi yaliyopokewa; hivyo سَجْدَةُ التّلاوَة (sajdatut-tilaawah) haihitajii *twahaarah.*

Hata hivyo, pamoja na kuwa si lazima mtu kuwa na udhu wakati wa kuleta sijda hiyo, lakini ni bora na ni jambo lenye kupendeza zaidi kama atakuwa ameshikamana na adabu za kusoma Qur-aan ambazo zinamtaka awe na udhu wakati wa kuisoma Qur-aan na anapokutana na Aayah ya sijda na kuiitika kwa kusujudu, atakuwa hana tatizo kwa kuwa tayari ana udhu wake, na Allaah Anajua zaidi.

[10] Al-Bukhaariy

**عَنْ الْأَسْوَدِ عَنْ عَبْدِ اللَّهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ أَنَّ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَرَأَ سُورَةَ النَّجْمِ فَسَجَدَ بِهَا فَمَا بَقِيَ أَحَدٌ مِنْ الْقَوْمِ إِلاَّ سَجَدَ فَأَخَذَ رَجُلٌ مِنْ الْقَوْمِ كَفًّا مِنْ حَصًى أَوْ تُرَابٍ فَرَفَعَهُ إِلَى وَجْهِهِ وَقَالَ: "يَكْفِينِي هَذَا" قَالَ عَبْدُ اللَّهِ: "فَلَقَدْ رَأَيْتُهُ بَعْدُ قُتِلَ كَافِرًا "**

**Imepokewa kutoka kwa Al-As-wad, kutoka kwa 'Abddullaah (رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ) kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisoma *Suwratun-Najm* akasujudu, basi hakubakia mtu katika kaumu (hata makafiri) ila alisujudu. Mtu mmoja akajaza kitanga cha mkono changarawe au mchanga akamwagia usoni mwake akisema: "Imenitosheleza hii" Akasema 'Abdullaah: "Nilikuja kumuona baada ya kuuliwa kuwa ni kafiri"[11]**

Suwrah pamoja na Aayah zake ambazo Muislamu hutarajiwa asujudu kwayo ni kama zifuatazo:

[11] Al-Bukhaariy

| No. | Suwrah | Namba ya Suwrah | Namba ya Aayah | No. | Suwrah | Namba ya Suwrah | Namba ya Aayah |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | الأعراف<br>Al-A'raaf | 7 | 206 | 9 | النّمل<br>An-Naml | 27 | 26 |
| 2 | الرّعد<br>Ar-Ra'd | 13 | 15 | 10 | السّجدة<br>As-Sajdah | 32 | 15 |
| 3 | النّحل<br>An-Nahl | 16 | 50 | 11 | ص<br>Swaad | 38 | 24 |
| 4 | الإسراء<br>Al-Israa | 17 | 109 | 12 | فصّلت<br>Fusswilat | 41 | 38 |
| 5 | مريم<br>Maryam | 19 | 58 | 13 | النّجم<br>An-Najm | 53 | 62 |
| 6 | الحجّ<br>Al-Hajj | 22 | 18 | 14 | الإنشقاق<br>Al-Inshiqaaq | 84 | 21 |
| 7 | الحجّ<br>Al-Hajj | 22 | 77 | 15 | العلق<br>Al-'Alaq | 96 | 19 |
| 8 | الفرقان<br>Al-Furqaan | 25 | 60 | | | | |